# MWONGOZO WA VIKAO VYA KUIMARISHA USHIRIKIANO KATI YA WIZARA, IDARA NA TAASISI ZISIZO ZA MUUNGANO ZA SERIKALI YA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA NA SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

**APRILI, 2019**

# YALIYOMO

**DIBAJI** .......... **III**

**SHUKURANI** .......... **V**

**1.0** Utangulizi .......... 1

**2.0** Malengo ya Vikao vya Kuimarisha Ushirikiano .......... 1

**3.0** Faida za Vikao vya Kuimarisha Ushirikiano .......... 2

**4.0** Muundo na Utaratibu wa Vikao vya Kuimarisha Ushirikiano .......... 2

**5.0** Ajenda za Vikao vya Kuimarisha Ushirikiano .......... 3

**6.0** Mawasiliano na Utaratibu wa Utoaji Taarifa .......... 3

**7.0** Utaratibu wa Kugharamia Vikao vya Kuimarisha Ushirikiano .......... 4

**8.0** Hitimisho .......... 4

# DIBAJI



Mhe. January Y. Makamba (MB)



Mhe. Mohamed A. Mohamed (MBM)

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni Muungano wa nchi zetu mbili ambao umekuwa ndio msingi mkuu wa amani na maendeleo yetu na umejengeka kwa umoja, mashirikiano, ushauriano na kuheshimiana. Ofisi ya Makamu wa Rais ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (SMT) na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) ukiondoa majukumu mengine kwa pamoja zina jukumu la kuratibu masuala yasiyo ya Muungano na kuhakikisha kuwa ushirikiano kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar unazidi kuimarika.

Ili kuendelea kudumisha Muungano wetu hatuna budi kuhakikisha kwamba tunazikabili kikamilifu na kwa wakati changamoto zilizopo na zinazojitokeza katika pande zote mbili za Muungano. Mwongozo huu unaeleza umuhimu wa vikao vya ushirikiano katika kushughulikia changamoto ili hatimae kuzipatia ufumbuzi muafaka.

Kutokana na kuzidi kuimarika kwa Muungano wetu kumeendelea kulileteа taifa letu sifa na heshima nyingi kutoka ndani na nje ya nchi yetu. Shime kwetu viongozi na watendaji wote kuhakikisha tunatekeleza majukumu yetu ipasavyo ili kuongeza tija na ufanisi

hatimae kuwaletea wananchi maendeleo. Tuna imani kuwa, mwongozo huu utasaidia kuimarisha ushirikiano baina ya pande mbili za Muungano.

***"Jukumu la Kudumisha Muungano ni la kila raia wa Tanzania"***



Mhe. January Y. Makamba (Mb.)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS - MUUNGANO NA MAZINGIRA (SMT)**



Mhe. Mohamed A. Mohamed (MBM.)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA PILI WA RAIS (SMZ)**

# SHUKURANI



Mhandisi Joseph K. Malongo



Ndg. Shaaban S. Mohamed

Kukamilika kwa maandalizi ya Mwongozo wa Vikao vya Kuimarisha Ushirikiano Kati ya Wizara, Idara na Taasisi Zisizo za Muungano za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (SMT) na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) ni matokeo ya juhudi za Viongozi na wataalam wa Ofisi ya Makamu wa Rais (SMT) na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais (SMZ) kuhakikisha kuwa kazi hii inakamilika na kuleta matunda yaliyokusudiwa.

Kwa namna ya kipekee tunapenda kutoa shukrani zetu za dhati kwa viongozi na watumishi wa Idara ya Muungano, Ofisi ya Makamu wa Rais (SMT) na Idara ya Uratibu wa Shughuli za Serikali, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais (SMZ) kwa juhudi na mshikamano wao katika kutekeleza majukumu yao ili kuhakikisha Muungano wetu unakua na kuimarika zaidi.


Mwisho, tunazishukuru wizara, idara na taasisi zisizo za Muungano za SMT na SMZ kwa ushirikiano wanaotoa katika kuimarisha uhusiano baina ya pande mbili za Muungano na hatimaye kukuza ustawi wa wananchi. Tukiwa watendaji wakuu tunaoratibu masuala

ya ushirikiano baina ya Serikali zetu, tunaamini mwongozo huu utatekelezwa kama inavyokusudiwa.



Mhandisi Joseph K. Malongo

**KATIBU MKUU**
**OFISI YA MAKAMU**
**WA RAIS (SMT)**



Ndg. Shaaban S. Mohamed

**KATIBU MKUU**
**OFISI YA MAKAMU WA**
**PILI WA RAIS (SMZ)**

# 1.0 Utangulizi

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iliundwa tarehe 26 Aprili, 1964 kwa Muungano wa Jamhuri ya Tanganyika na Jamhuri ya Watu wa Zanzibar. Kwa mujibu wa katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 Ibara ya 34 (1) inaeleza kuwa "kutakuwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo itakuwa na mamlaka juu ya mambo yote ya Muungano katika Jamhuri ya Muungano, pia juu ya mambo mengine yote yahusuyo Tanzania Bara". Aidha, kwa upande wa Zanzibar, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) itakuwa na mamlaka ya kushughulikia mambo yote yasiyo ya Muungano kwa upande wa Tanzania Zanzibar.

Ofisi ya Makamu wa Rais (SMT) na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais (SMZ) zimeandaa mwongozo maalum wa vikao vya kuimarisha ushirikiano kwa lengo la kuziwezesha Wizara, Idara na Taasisi husika kujiandaa na kushiriki kikamilifu katika vikao vya ushirikiano ili kuhakikisha utekelezaji wa majukumu yao unazingatia mahitaji ya pande mbili za Muungano.

# 2.0 Malengo ya Vikao vya Kuimarisha Ushirikiano

Malengo ya vikao vya kuimarisha ushirikiano ni kama ifuatavyo:-

i. Kubadilishana uzoefu, sera, sheria, utaalamu na wataalamu kati ya SMT na SMZ;
ii. Kuimarisha ushirikiano wa kiutendaji na ziara za kikazi za mara kwa mara kati ya sekta zinazofanya shughuli zinazoshabihiana; na
iii. Kujadili na kushughulikia changamoto mbalimbali zilizopo na zitakazojitokeza katika Muungano.

## 3.0 Faida za Vikao vya Kuimarisha Ushirikiano

Kuna faida nyingi zinazotokana na vikao vya ushirikiano baina ya Wizara, Idara na Taasisi za pande mbili za Muungano. Faida hizo ni pamoja na:-

i. Kubainisha changamoto, kuzijadili na kuzitafutia ufumbuzi wa kudumu;
ii. Viongozi na watendaji kuwa na uelewa na msimamo wa pamoja kuhusu masuala ya kisekta ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;
iii. Viongozi na wataalam kufahamiana na kujenga misingi bora ya ushirikiano;
iv. Kuhuisha sheria, kanuni, taratibu na miongozo inayohusu Wizara, Idara na Taasisi zisizo kuwa za Muungano kwa lengo la kuboresha maeneo yenye changamoto;
v. Kuendeleza jitihada za kutambua mahitaji na matarajio ya wananchi;
vi. Kuendelea kukabiliana na changamoto zinazotokana na mabadiliko ya mfumo wa uchumi duniani; na
vii. Kujenga msimamo wa pamoja kuhusu fursa za uhusiano na ushirikiano wa kikanda na kimataifa.

## 4.0 Muundo na Utaratibu wa Vikao vya Kuimarisha Ushirikiano

Muundo wa vikao vya kuimarisha ushirikiano utakuwa na ngazi zifuatazo:-

i. Mawaziri;
ii. Makatibu Wakuu; na
iii. Wataalam.

Wizara, Idara na Taasisi zisizo kuwa za Muungano za pande zote mbili za Muungano zinatakiwa kufanya vikao vya ushirikiano

visisivyopungua viwili kwa mwaka. Vikao vyote vitaanza na mikutano ya Wataalam, Makatibu Wakuu na Mawaziri. Utaratibu wa uendeshaji wa vikao hivi utazingatia ngazi husika. Kwa mfano, kikao cha Mawaziri, mwenyekiti atakuwa ni Waziri wa upande/sehemu kikao kinapofanyika akisaidiana na mwenyekiti mwenza ambaye ni Waziri toka upande mwingine wa Muungano. Aidha, vikao vya Makatibu Wakuu na ngazi ya Wataalam vitafuata utaratibu huo huo. Pande zote mbili zitashiriki kikamilifu kuanzia hatua za awali.

**TANBIHI:** Katika kila ngazi ya vikao hivyo ni lazima kuwe na mjumbe kutoka Ofisi ya Makamu wa Rais (SMT) na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais (SMZ).

## 5.0 Ajenda za Vikao vya Kuimarisha Ushirikiano

Ajenda za vikao vyote vya kuimarisha ushirikiano zitatakiwa kuandaliwa na sekretarieti ya wataalamu ambao watakuwa wameteuliwa na wizara, idara na taasisi husika. Sekretarieti hiyo isizidi wajumbe sita watatu kutoka SMT na watatu SMZ. Kazi za Sekretarieti zitakuwa ni kama ifuatavyo:-

i. Kuibua ajenda;
ii. Kuandaa kikao;
iii. Kuandaa taarifa ya kikao; na
iv. Kufuatilia utekelezaji wa makubaliano ya kikao.

Aidha, Sekretarieti hiyo iwe ni ya kudumu ili kuwa na mtiririko mzuri wa taarifa zilizojadiliwa.

## 6.0 Mawasiliano na Utaratibu wa Utoaji Taarifa

Ratiba ya vikao vya ushirikiano itaandaliwa na Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kushirikiana na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais na

kusambazwa katika Wizara, Idara na Taasisi husika.

Baada ya vikao hivyo kufanyika taarifa ya vikao iwasilishwe katika ofisi hizo si zaidi ya wiki mbili baada ya kikao kwa ajili ya rejea. Aidha, Wizara, Idara na Taasisi zisizo za Muungano za pande mbili zinapofanya mawasiliano zina wajibu wa kutoa taarifa Ofisi ya Makamu wa Rais na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ambazo zina dhamana ya kuratibu masuala yasiyo ya Muungano.

## 7.0 Utaratibu wa Kugharamia Vikao vya Kuimarisha Ushirikiano

Bajeti ya kikao (ukumbi, chakula na shajala) itagharamiwa na upande ulioandaa kikao na vikao hivi vifanyike kila upande wa Muungano kwa kubadilishana.

## 8.0 Hitimisho

Ufanisi wa vikao vya kuimarisha ushirikiano unategemea juhudi na dhamira za dhati za viongozi na watendaji wa pande zote mbili za Muungano ili kufikia malengo yanayokusudiwa. Ofisi ya Makamu wa Rais (SMT) na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais (SMZ) zinatarajia kuwa mwongozo huu utatumika kama nyenzo na dira muhimu katika kuhakikisha ushirikiano baina ya pande mbili za Muungano unazidi kukua na kuimarika ili wananchi waweze kunufaika na fursa za kimaendeleo zinazojitokeza.



*Mwalimu Julius Kambarage Nyerere (kushoto) na Sheikh Abeid Amani Karume wakibadilishana Hati za Muungano wa Tanganyika na Zanzibar tarehe 27 Aprili, 1964.*